

Uwanachama na Idara ya Kujislihisha

Uwanachama Upya. Membership and Capital Subscriptions Unit of the Corporate Secretariat [Idara ya Ofisi ya Uendeshaji ya Uwanachama na Kujisalihisha] ni mojawapo ya sehemu ya kwanza ya kuelekeza maswali kuhusu uwanachama upya katika World Bank Group [Mshikano wa Benki]. Mshikano wa Benki inahusisha mashirika matano: International Bank for Reconstruction and Development (IBRD) [Benki ya Kimataifa ya Marekebisho na Maendeleo], International Development Association (IDA) [Shirikisho la Kimataifa la Maendeleo], International Finance Corporation (IFC) [Muungano wa Kimataifa wa Fedha], Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA) [Shirika la Uthibiti wa Uwekezaji], na International Centre for the Settlement of Investment Disputes (ICSID) [Kituo cha Kimataifa cha Utatuzi wa Mizozo ya Uwekezaji].

Idara ina jukumu la mawasiliano ya kwenda na kutoka kwa nchi inayofanya maombi kuhusu desturi za uwanachama, kama vile kiwango cha kujisalihisha na malipo yanayotakiwa na waraka wake. Huandaa chapisho la uwanachama na ripoti inayotilia mkazo kukubaliwa ombi lenye sheria zinazohusu uwanachama wa nchi kwa Bodi la Uendeshaji, na Bodi inapokubali, hadi kwa Bodi za Magavana kwa upigaji kura.

Idara husimamia kura ya Magavana kwa barua, shughuli ambayo huchukuwa mda wa wiki sita kukamilika. Kura za Magavana hupelekwa hadi Ofisi ya Uendeshaji kwa barua ya kawaida, barua ya ushindikizi, telex ama fax, na zina rikodiwa katika orodha ya kuraitakayo idhinishwa na Wakurugenzi Watendaji muda wa kupiga kura unapofikia mwisho.

Hali ya Uwanachama. Idara ndiyo hifadhi ya taarifa za Mshikano wa Benki zenye kushughulikia hali ya maombi ya uwanachama, tarehe za kuanza uwanachama, tarehe za kutia sahihi kwa Vifungo vya Makubaliano za IBRD/IDA/IFC, na Makubaliano za MIGA/ICSID, na tarehe za kupeanwa vyombo vya kuratibiwa kwa kukubaliwa kwa Vifungo vya Makubaliano za IBRD/IDA/IFC na Makubaliano za MIGA/ICSID.

Majina Rasmi ya Nchi. Idara, ikishirikiana na Idara ya Sheria, huamua utumizi wa majina sahihi ya nchi wanachama, na hutoa taarifa panapo tokea mabadiliko. Uhifadhi orodha ya nchi wanachama pamoja na maandishi yaliyokubaliwa kwa majina ya nchi, pamoja na vifupisho vyake; orodha inapatikana katika Mtandao wa ndani kwa ndani wa Mshikano wa Benki.

Hifadhi za Rikodi za Uwanachama. Records Management Division of the Corporate Secretariat [Idara ya Usimamizi wa Rikodi ya Ofisi ya Uendeshaji] ndiyo yenye kuhifadhi rekodi zote rasmi zinazo husika na uwanachama katika Mshikano wa Benki. Rikodi hizi hujumuisha nakala rasmi za Vifungo vya Makubaliano vya IDA na IFC, na Makubaliano za MIGA na ICSID. Hata hivyo, ingawa Seriakali ya Marekani ndiyo muhifadhi rasmi wa Vifungo vya Makubaliano vya IBRD, nakali rasmi inahifadhiwa katika United States Department of State [Idara ya Mambo ya Nje ya Marekani].

Waraka zinazopelekewa Mshikano wa Benki. Kama vile nakala za sheria zinazo peana ruhusa kwa nchi, uwezo kamili, vyombo vya makubaliano, na thibitisho la malipo ya uwanachama, pia huhifadhiwa katika Records Management Division of the Corporate Secretariat [Idara ya Usimamizi wa Rikodi ya Ofisi ya Uendeshaji]. Nakala za waraka hizi zinapatikana kwa maombi.